# ULINGANISHI WA MUUNDO WA VITOMEO KATIKA KAMUSI MBILI ZA KISWAHILI - KIINGEREZA.

E.K.F Chiduo

*Ikisiri*

Ulinganishi wa Kamusi Sanifu ya Kiswahili-Kiingereza (KSKK, 1993) na Kamusi ya Kiswahili- Kiingereza (KKK, TUKI 2001) unazingatia mtazamo wa Nkweti-Azel. Mtizamo huu unazingatia vipengelele vikuu vinane vilivyogawanyika katika vipengele vidogo 21:

(i) Otografia ( Kitomeo, kibadala, kisawe)
(ii) Fonolojia (matamshi)
(iii) Mofolojia na Sintaksia (viambiasi wingi, ngeli za nomino, vinyambuo, uelekezi)
(iv) Kategoria za maneno
(v) Pragmantiki (tahadharia ya matumizi alama za rejesta za kijiografia)
(vi) Etimolojia (asili, maneno husiani)
(vii) Fasiri (fasiri ya maneno, mifano muktadha)
(viii) Uhusiano (Kinyume, maneno husiani)

Ulinganishi huu unaonesha kuwa, KSKK iliingiza vipengele vidogo 14 na kuacha 7 wakati KKK iliingiza vipengele vidogo 12 na kuacha 9. Ni KKK tu iliyoingiza taarifa za ngeli za nomino na uelekezi.

## 1.0 Utangulizi

Hadi sasa, kuna kamusi thaniya kadhaa za Kiswahili-Kiingereza zilizopata kuchapishwa kwa ajili ya matumizi ya jumla. Lengo la makala hii ni kufanya uchambuzi wa ulinganifu wa muundo wa vitomeo wa kamusi mbili yaani **Kamusi Sanifu ya Kiswahili – Kiingereza** (KSKK) (Frederick Johnson 1939, na ile ya **Kiswahili–Kiingereza** (KKK) (TUKI 2001). Uchambuzi utazingatia vipengele mbalimbali vya muundo wa vitomeo katika kamusi hizi mbili kwa kutumia mtazamo wa Nkwenti – Azeh (1995) ambao umetumia vipengele vikuu vinane vinavyohusiana na muundo wa kitomeo. Vipengele hivyo ni otografia, fonolojia, mofolojia, kategoria za maneno, pragmatiki, etimolojia, fasiri, na uhusiano. Vipengele hivi vikuu vina jumla ya vipengele vidogo kumi na tisa. Mtazamo wa Nkwenti–Azeh umetumiwa na Pedro A.Fuertes Olivera na Marisol Velesco Sacristan katika kuchambua na kulinganisha kamusi za uchumi za Kihispania - Kiingereza, na Kiingereza - Kihispania. Kwa kutumia mtazamo huu waligundua kuwa baadhi ya vipengele muhimu vilikuwa vimeachwa na hivyo kupendekeza kuingizwa katika matoleo ya baadaye ya kamusi hizo. Uchambuzi wa kamusi za KSKK na KKK utafanywa kwa kutumia vipengele ishirini kwani vipengele viwili vya visawe kamili na visawe hafifu vimeunganisha na kuwa na kipengele kimoja cha visawe. Pili kuna vipengele viwili vimeongezeka ambavyo ni kipengele cha ngeli za nomino na kipengele cha uelekezi; vipengele hivi

havikutumiwa na Nkwenti - Azeh na hivyo vinafanya idadi ya vipengele vidogo kuwa ishirini.

Matokeo ya uchambuzi wa kamusi hizi mbili za Kiswahili-Kiingereza utasaidia kubainisha vipengele muhimu vinavyopaswa kuzingatiwa na kuingizwa ndani ya kamusi katika matoleo mengine au kamusi mpya za Kiswahili-Kiingereza zitakapokuwa zinatayarishwa.

## 2.0 Kamusi zilizochambuliwa

### 2.1 Kamusi Sanifu ya Kiswahili – Kiingereza [(KSKK) (1939)]

Kamusi hii ndiyo kamusi pekee ya Kiswahili- Kiingereza ya kiwango cha juu iliyotumiwa na watumiaji wa kamusi wa jumla kwa miaka mingi tangu ilipochapishwa mara ya kwanza mwaka 1939. Hadi kufikia mwaka 2000 kamusi hii ilikuwa imerudiwa kuchapwa mara 45. Inakadiriwa kuwa Kamusi hii ina vitomeo takribani 20,000. Tangu ilipochapishwa kwa mara ya kwanza kamusi hii haijafanyiwa marekebisho.

Kufikia mwaka 2001 kamusi hii ilikuwa ndiyo kamusi pekee iliyokuwa katika chati ya juu kwa watumiaji mbalimbali wakiwamo walimu, wanafunzi, wafasiri na wataalam wengine wa lugha hapa Tanzania na nchi za nje.

### 2.2 Kamusi ya Kiswahili – Kiingereza [(KKK) (2001)]

Kamusi hii imetolewa baada ya miaka takribani 60 kupita tangu kamusi ya Kiswahili – Kiingereza ya Frederick Johnson kuchapishwa. Kamusi ya Kiswahili - Kiingereza ya TUKI ilianza kusawidiwa mwezi January 1997 na kukamilika mwaka 2000. Kamusi hii ina vitomeo takribani 30,000 (TUKI 2001).

## 3.0 Matokeo ya uchambuzi kwa mujibu wa vipengele vya ulinganishi.

### 3.1 Matokeo kwa Ujumla

Uchambuzi kwa mujibu wa vipengele vya ulinganishi vya Nkwenti – Azeh (1995) kwa Kamusi za Kiswahili- Kiingereza umefanywa na matokeo yake yameonyeshwa katika viwango vitatu. Kama kipengele fulani kimeshughulikiwa katika kamusi huonyeshwa kwa 'Ndiyo' na kama hakikushughulikiwa kabisa huonyesha kwa 'Hapana'. Iwapo kipengele kimeshughulikiwa kwa uchache sana chini ya asilimia 10 huonyeshwa kwa 'Kidogo'. Kwa mfano katika KKK vibadala vilivyoingizwa havizidi asilimia 2 ya vidahizo vyote na hivyo imeashiriwa kwa neno 'Kidogo'. Yafuatayo ni matokeo ya uchambuzi huu:

| Kategoria ya Taarifa | | KKK 2001 | KSKK 1939 |
|---|---|---|---|
| (i) | **Otografia** | | |
| (a) | Kitomeo (Kidahizo) | Ndiyo | Ndiyo |
| (b) | Kibadala | Kidogo | Ndiyo |
| (c) | Sinonemia (Kisawe) | Hapana | Ndiyo |
| **(ii)** | **Matamshi** | Hapana | Hapana |
| **(iii)** | **Mofolojia Sintaksia** | | |
| (a) | Viambishi vya wingi | Ndiyo | Ndiyo |
| (b) | Ngeli za Nomino | Ndiyo | Hapana |
| (c) | Vinyambuo | Ndiyo | Ndiyo |
| (d) | Uelekezi | Ndiyo | Hapana |
| **(iv)** | **Kategoria za Maneno** | Ndiyo | Ndiyo |
| **(v)** | **Pragmatiki** | | |
| (a) | Tahadhari za matumizi | Ndiyo | Ndiyo |
| (b) | Alama za rejesta | Hapana | Hapana |
| (c) | Alama za kijiografia | Hapana | Hapana |
| (d) | Utangamano | Hapana | Ndiyo |
| **(vi)** | **Etimolojia** | | |
| (a) | Asili | Ndiyo | Ndiyo |
| (b) | Maneno Husiani | Hapana | Ndiyo |
| **(vii)** | **Fasiri** | | |
| (a) | Fasiri ya maneno | Ndiyo | Ndiyo |
| (b) | Mifano / Muktadha | Ndiyo | Ndiyo |
| (c) | Alama za Uwanda Maalum | Kidogo | Hapana |
| **(viii)** | **Uhusiano** | | |
| (a) | Kinyume | Hapana | Hapana |
| (b) | Maneno husiani | Hapana | Ndiyo |

Uchanganuzi wa data unaonyesha kuwa KKK imeingiza vipengele 10 (50%) imeacha vipengele 8 (40%), vipengele 2 (20%) vimeingizwa kidogo. KSKK imeingiza vipengele 13 (65%) na imeacha vipengele 7 (35%). Katika kamusi hizi vipengele 8 vimelingana yaani kwa asilimia 40% kamusi hizi zinalingana kwa kuingiza vipengele vya "ndiyo" vinavyofanana. Kwa asilimia 15 zinalingana kwa kuwa na vipengele vya "hapana" vinavyofanana. Kwa asilimia 10 KKK ina vipengele vya "ndiyo" vinavyotofautiana na vya KSKK yenye asilimia 20 ya vipengele vya "ndiyo" vinavyotofautiana na KKK. Uchambuzi huu unaonyesha kuwa KKK ina vipengele viwili vya Kidogo ambapo KSKK haina kipengele cha kidogo. Hii inaweza kudokeza kuwa wanakamusi wa KKK waliingiza vipengele hivi bila kukusudia ambapo katika KSKK vipengele hivyo vimeingizwa au havikuingizwa kabisa.

### 3.1.1 Otografia

Katika kipengele cha otografia vipengele vidogo vitatu vimejadiliwa; yaani vitomeo, vibadala na visawe.

#### 3.1.1.1 Vitomeo

Kitomeo kimefasiriwa kuwa ni "aya ndogo katika Kamusi ambayo ina kidahizo na taarifa zote zinazohitajika kukifafanua." (TUKI 2001:x) Mifano ya vitomeo kutoka kamusi zinazochambuliwa.

(i) **mganga** nm wa- *[ a-/wa-]* medical person, doctor: ~ *Mkuu* Doctor Incharge; ~ *wa kienyeji* traditional Healer, herbalist; ~ *wa farasi* farrier.(KKK, uk.200)

(ii) **Mganga,** n. wa-. See under Ganga (KSKK, uk. 277)

(iii) **Ganga,** v blind up, fasten together, splice, mend (what is injured or broken). Hence esp- of doctor's work generally, 'apply remedy, cure heal'. *Ganga mguu* put a leg in splints. *Ganga jeraha* bandage a wound. *Ganga tumbo* attend to the stomach. Ps. Gangwa.St. Gangika. Prep. Gangia. Cs. Gangisha. Rp. Gangana. CV Gangua, v. (1) same as ganga, v.; (2) save, get out of a difficulty, set free from a charm. Mganga, n. wa- a native doctor, medicine man. ( KSKK, 1939: 111)

Kuna tofauti kadhaa zinazobainisha kati ya vitomeo hivi. Tofauti mojawapo ipo katika herufi ya kwanza ya kidahizo. Kidahizo katika KSKK huanza kwa herufi kubwa, ambapo katika KKK huanza kwa herufi ndogo isipokuwa kwa majina maalum tu kama yanayotaja jina la Mwenyezi Mungu kama Mola, Jalali, Allah n.k. Utaratibu wa kidahizo kuanza na herufi ndogo umekuwa ndiyo kaida inayofuatwa na kamusi nyingi ikiwa na pamoja na *Oxford Advanced Learner's Dictionary* (1995), *Kamusi ya Visawe* (Mohammed na Mohammed 1998), *Modern Swahili – Modern English* (Baba Malaika 1991), *Webster's New World Dictionary* (1971), *Kamusi ya Kiingereza - Kiswahili* (TUKI 1996) na nyingine nyingi. Pia katika kamusi zote hizo zilizotajwa kidahizo kimeonyeshwa kwa wino mzito na kwa kufuata mpangilio wa alfabeti.

#### 3.1.1. 2 Vibadala

Kibadala ni neno moja lakini lina namna mbili au zaidi za kuliandika. KSKK imeingiza vibadala vingi ikiwa ni mbinu ya kutolea fasiri kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo:

| | |
|---|---|
| **Kapatula**, n. see Kaputula | (KSKK,uk 173) |
| **Kidei,** n. see Kideri | (KSKK,uk.188) |
| **Maksusi.*** see mahsusi under Hususa | (KSKK,uk. 256) |

Katika uchambuzi uliofanywa kuhusu kipengele hiki herufi A na B za kamusi hizi mbili zimechambuliwa. Matokeo yanaonyesha kuwa katika KKK ni vitomeo 11 tu kati ya vitomeo 1050 (1.8%) ndivyo vimeonyesha kuwa na vibadala. Uingizaji wa vibadala hivyo unaonyesha kuwa maana au maelezo yametolewa pande zote yaani

kila kibadala kimeingizwa kama kidahizo na kimepewa maelezo yake kamili kama katika mifano ifuatayo:

| | |
|---|---|
| **ahsante!*** | pia **asante!** *ki* Thanks! Thank you.(KKK, uk.5) |
| **asante!*** | *ki* thank you: ~ sana Thank you very much.(Kar) (KKK, uk. 14) |
| **bindo** | pia **kibindo** *nm* a folded part of loincloth usually used as pocket for carying things.(KKK, uk. 27) |
| **kibindo** | nm vi- [ ki-/ vi-] fold/ knot of the loin cloth, used as pocket. (KKK uk. 135) |

Katika KSKK kwa herufi A & B kuna vitomeo 59 vyenye vibadala kati ya vitomeo 645 vilivyomo katika herufi hizo mbili, sawa na asilimia 9.0. Uingizaji huu wa vibadala unatofautiana na uingizaji ulivyofanywa katika KKK kwani katika KSKK maelezo yametolewa katika kitomeo kimoja tu kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

**Anjili,*** n. See Injili. (KSKK, uk. 17)
**Injili,*** n.the new testament. (KSKK, uk. 143)

**Askafu,*** n. ma- See **Askofu.** (KSKK, uk. 20)
**Askofu,*** n ma- a bishop. (KSKK, uk 20)

KSKK imeingiza vibadala vingi kuliko KKK. Hii inaweza kuwa imetokana na ukweli kuwa wakati ilipokuwa inatayarishwa ndiyo wakati juhudi za kusanifisha Kiswahili zilipokuwa zimeanza na hivyo kuruhusu mbili au zaidi za kuandika neno moja kuingiza katika kamusi. Pia kuna uwezekano kuwa mwaka 1997, wakati KKK ilipokuwa inatayarishwa baadhi ya maneno yaliyokuwa na vibadala hayakuwa na matumizi makubwa na hivyo yakaachwa na matokeo yake ni kupungua sana kwa vibadala katika KKK. Katika herufi hizo mbili zilizofanyiwa uchunguzi imedhihirika kuwa vibadala vingi vimetokana na maneno toka lugha za kigeni hususan Kiarabu. Hii inadokeza kuwa maneno hayo yaliingizwa katika Kiswahili yakiwa na maumbo tofauti katika maeneo tofauti ya wazungumzaji wa Kiswahili. Vibadala katika kamusi si jambo baya kwani vinasaidia kutoa picha ya historia ya maendeleo ya kukua kwa lugha.

### 3.1.1.3 Visawe

Visawe ni maneno mawili au zaidi yenye maana moja (Harris 1973; Singh 1982; Jackson 1988). Maneno mawili yanaweza kuwa visawe kamili kama tu yanaweza kubadilishana nafasi katika muktadha mmoja bila kubadili maana (Singh 1982:61).

Katika KKK visawe vya Kiswahili havikuingizwa katika kitomeo kimoja, ambapo katika KSKK visawe vimeingizwa kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo:

**Nyenyere,** n a kind of very small black ant, also called *sisimizi*.
(KSKK, uk. 345)

**Sisimizi,** n. a small black harmless ant. (Cf. **nyenyere**) (KSKK, uk. 433)

**Nyenze,** n. a cricket, also called ***nyenje, chenene.*** (KSKK, uk. 345)

**Nyenje,** n. a kind of cricket, also called ***chenene, nyenze*** (KSKK, uk.345)

**Chenene,** n. a kind of a large cricket that makes a screening noise at night; It burrows into the ground. (Cf.**nyenze, nyenje**) (KSKK, uk. 54)

**Kafila,*** n. a caravan.(Rarely heard for common ***msafara*** and ***safari*** (KSKK, uk.165)

Manufaa ya kuyahusisha maneno ambayo ni visawe kama ilivyo katika KSKK ni kwamba msomaji hupata uhusiano baina ya maneno hayo papohapo. Katika KKK, maneno nyenyere na sisimizi yameingizwa katika vitomeo tofauti bila ya kuonyesha mahusiano yaliyopo baina yao kama inavyoonyesha hapa chini:

**nyenyere** nm [*a-/wa-*] tiny black ant (KKK, uk.249)
**sisimizi** nm [a-/ wa-] small black ant (KKK, uk 297)

Fasiri zilizotolewa kwa kila kitomeo zinadhihirisha kuwa maneno haya kwa kiwango fulani yana maana moja yaani ni visawe. **Hata** hivyo itamchukua muda mwanafunzi wa Kiswahili kuweza kupata neno la pili baada ya kufahamu mojawapo kwanza. Kamusi haikuweza kuyahusianisha moja kwa moja katika kitomeo kimoja tofauti na yalivyoonyeshwa kwenye KSKK. Katika kamusi nzima ya KKK hakuna hata kitomeo kimoja kilichoingiza visawe.

### 3.2 Matamshi

Kamusi zote mbili hazikuonyesha matamshi ya vidahizo. Hii ni kwa sababu maneno mengi ya Kiswahili hutamkwa kama yanavyoandikwa. Hivyo kipengele cha matamshi hakikushughulikiwa. Hata hivyo kungekuwa na manufaa zaidi kwa mtumiaji wa kamusi za Kiswahili – Kiingereza kama baadhi ya maneno yangewekewa matamshi hususan yale yaliyoingia kwenye Kiswahili kutoka lugha nyingine. Mfano baadhi ya maneno yaliyotokana na Kiarabu yana sauti ambazo maandishi yake ni tofauti na yanavyotamkwa. Mfano, sauti /ð/ katika maneno kama *dhahabu*, *dhambi* na *dhiki*. Sauti /θ/ kama katika maneno *thamani* na *thumuni*., Sauti /ŋ/, kama katika maneno *ng'ambo* na *ng'ombe*. Kwa kuwa maneno yanayoambatana na sauti hizi yanawapa taabu ya utamkaji hususan wanaojifunza Kiswahili hivyo ni muhimu kuonyesha matamshi yake ili kuwarahisishia kujifunza matamshi ya maneno hayo.

### 3.3 Mofolojia

#### 3.3.1 Kanuni za kimofolojia

Katika kipengele cha mofolojia mabadiliko ya maneno kufuatana na kanuni za kimofolojia ya Kiswahili imetumika kama kipengele kimojawapo cha ulinganishi. Mojawapo ya kanuni za kimofolojia ya Kiswahili ni maumbo ya wingi. Baadhi

ya nomino za Kiswahili huwa na kiambishi awali cha wingi. Pia unyambulishi wa vitenzi ni kanuni mojawapo ya kimofolojia. Vitenzi vya Kiswahili vina uwezo wa kunyambuka na kuzalisha vitenzi vingine au nomino kama mifano ya hapa chini inavyoonyesha:

| **Kitenzi** | **Nomino** |
|---|---|
| linda | lindo |
| jenga | ujenzi |
| lima | kilimo |

| **Kitenzi** | **Kitenzi** |
|---|---|
| penda | pendana |
| piga | pigania |
| enda | endesha |

Katika KSKK, nomino zinazotokana na vitenzi maana zake zimetolewa katika kidahizo cha kitenzi na kidahizo cha nomino hurejeshwa kwenye kidahizo cha kitenzi kama katika mifano ifuatayo:

**Lindo,** n. *ma-*. See under Linda.(KSKK, uk. 247)
**Linda,** v.(1) defend, protect,guard,watch, keep safe; (2) keep off, fend off,guard against, watch for
**Lindo,** n. ma- watching place, station, post (to guard)... (KSKK, uk.247)

**Mchinjaji,** n. wa- See under Chinja. (KSKK, uk.271)
**Chinja,** v. (Mombasa, tinda) (1) slaughter, cut the throat of, kill- esp. of killing for food ...
**Mchinjaji,** n. wa- a butcher, a slaughterer ...(KSKK, uk. 56-57)

Katika KKK vidahizo vyote hupata fasiri zake kamili pande zote kama inavyoonyeshwa kwenye mifano ifuatayo:

**chinj.a** *kt* [*ele*] 1 slaughter, slay, cut the throat. 2 Kill ruthlessly. 3 cut level the rim of a clay vessel in making it.(*tde*) chinjia; (*tdk*) chinjika; (*tdn*) chinjana; (tds) chinjisha; (tdw) chinjwa. machinjioni *nm*. (KKK, uk.46)
**mchinjaji** *nm* wa- [*a-/wa-*] butcher; slaughterer. (KKK, uk. 194-95)

**chum.a** *kt* (*ele*) 1 pick, pluck, gather from a tree (flower or fruit). 2 make money, earn: ~ fedha earn money: (*tde*) chumia; (*tden*) chumiana; (*tdk*) chumika; (*tds*) chumisha; (*tdw*) chumwa. (KKK,uk.51).

**chumo** *nm* [*i-/zi-]* 1 plucking. 2. produce, yield, profit, gain, income.(KKK,uk.51)

Tofauti ya wazi kati ya kamusi hizi mbili kuhusu kipengele hiki ni kuwa KSKK imeonyesha kwa uwazi mahusiano ya nomino zinazotokana na vitenzi kwa kurejesha fasiri za nomino hizo kwenye vitomeo vya vitenzi. KKK haikuonyesha moja kwa moja uhusiano huo kwani kila kidahizo kimepewa fasiri zake kamili.

KKK inamrahisishia mtumiaji wa kamusi kupata maana ya neno moja kwa moja bila mzunguko ndani ya kamusi. Hata hivyo KSKK inamwezesha mtumiaji wa kamusi hiyo kuelewa mahusiano yaliyopo baina ya maneno.

### 3.3. 2 Unyambulishi .

Katika kamusi zote unyambulishi wa vitenzi umeonyeshwa. Katika KKK unyambulishi umeonyeshwa kwa ukamilifu wake na vifupisho vyake vimeonyeshwa kwa Kiswahili kama katika mifano ifuatayo:

**engu.a** kt [ele] skim, take scum off water/milk etc. (tde) engulia; (tden) enguliana; (tdew) enguliwa; (tdk) enguka; (tdn) enguana; (tds) engusha. (KKK, uk.67)

**iv.a kt** [*sie*] 1 ripen, be ripe; mature. 2 be ready to be eaten;be cooked: *Nyama ime~* the meat is cooked. 3 be ready for something which was being prepared: *Mambo yame~* things are ready. (nh) ~ uso feel pain, feel shame. (tde) **ivia**; **(tdk)** ivika; (tds) ivisha. (KKK, uk. 112).

**fufu.a** kt [ele] 1 resurrect. 2 revive, recall regenerate, revamp: ~ *deni* revive a debt. (tde) fufulia; (tdew) fufuliwa; (tdk) fufuka; (tdn) fufuana; (tds) fufusha. (KKK, uk. 76)

Katika KSKK vinyambuo vimeonyeshwa kwa mtindo tofauti kama katika mfano ufuatao:

**Fufua, v.** cause to revive, bring to life again, resuscitate, restore revive. *Fufua maiti* bring a dead body to life. *Fufua mgonjwa, give* strength to an invalid. *Fufua deni* bring up a forgotten debt. *Fufua desturi (sheria, chama)*, revive a custom (Law association or guild). St. Fufuka. Prep. Fufulia. Cs. Fufusha. (KSKK, uk. 99-100)

Katika kipengele hiki tofauti zinazojitokeza ni kuwa KKK imeonyesha vinyambuo vyake kwa kifupi na kwa Kiswahili ambapo KSKK imeonyesha vifupisho vya vinyambuo kwa Kiingereza. Hata hivyo katika KSKK baadhi ya vitenzi vinyambuo vyake havikuonyeshwa (Linganisha mfano wa fufua).

### 3.3.3 Viambishi vya wingi

Kamusi zote mbili zimeonyesha viambishi vya wingi kwa kila nomino yenye kiambishi cha wingi kama katika mifano ifuatayo:

**lindo,** n. *ma-*. See under linda.(KSKK, uk. 247

**limbuko** *nm ma-* [*li-/ya-*] first taste/experience of th.(KKK,uk.174).

**kidundu,** n. *vi-*. The forehead. (Cf *kipaji* ) (KSKK, uk. 189)
**kipimio** nm *vi-* [*ki-/vi-*] scale. (KKK, uk. 148)

Katika mifano hii, maumbo *ma-* na *vi-* ni viambishi vinavyoashiria wingi katika vidahizo hivyo.

**3.3.3.1 Ngeli za Nomino**

Lugha ya Kiswahili huzigawa nomino katika makundi yanayoitwa ngeli za nomino kwa kila kidahizo ambacho ni nomino. KKK imeingiza ngeli zote za nomino katika mtindo ufuatao:

**gurudumu*** *nm ma-* [*li-/ ya-*] wheel: ~ *la samani* castor. (Kaj) (KKK, uk.93)

**mgunduzi** *nm wa-* [*a-/wa-*] discoverer, inventor. (KKK, uk.201)

Katika mifano hii, neno **gurudumu** limo katika kundi la ngeli ya [*li-/ya-*] na neno mgunduzi limo katika ngeli ya [*a-/wa-*]. Uonyeshaji wa makundi ya ngeli kwa kila nomino iliyoingizwa katika Kamusi kunamwelekeza mtumiaji wa Kamusi hususan mwanafunzi wa Kiswahili katika matumizi sahihi ya maneno katika kufanya upatanisho wa kisarufi wa nomino husika. KSKK haikuingiza ngeli za nomino na huo ni upungufu kwani haimwongozi mwanafunzi wa Kiswahili katika kutunga sentensi sahihi.

**3.3.3.4 Uelekezi**

Uelekezi ni dhana inayohusiana na uwezo wa kitenzi kung'oeka vipashio vingine (Kihore na wenzake 2001). KKK inaonyesha kanuni hizi muhimu za vitenzi vya Kiswahili kwa kuonyesha kama kitenzi ni elekezi yaani kinachukua yambwa, au kama kitenzi si elekezi kwa maana kuwa hakichukui yambwa. Maneno engua na iva hapo juu yanaweza kutofautishwa kwa sifa ya uelekezi kwani engua ni elekezi [ele] yaani kina uwezo wa kung'oeka vipashio vingine; yaani, kitenzi engua kinaweza kufuatiwa na kikundi nomino (KN), na kitenzi iva sielekezi [sie] kwa kuwa hakina uwezo wa kung'oeka vipashio vingine. KSKK haikukishughulikia kipengele hiki.

**3.3.4 Kategoria za maneno**

Kwa kawaida kamusi karibu zote huonyesha kategoria za maneno. Hata zile kamusi ndogo za watoto zinazojitahidi kuepuka kuwapa watoto mambo mengi yahusuyo lugha ya kikamusi haiwezi kukwepa kuwaonyesha kategoria za maneno kwani hili ni jambo la msingi kabisa katika kusawidi kamusi yoyote ile. Kwa mfano kamusi ya watoto iitwayo *Children's Dictionary* imeonyesha kategoria za maneno. Hata hivyo baadhi ya Kamusi hazikuonyesha kategoria za maneno. Kamusi ya *Junior English – Swahili Dictionary* ni mfano mmoja wa aina hiyo. Kwa kutoonyesha kategoria za maneno, kamusi za namna hii zinapunguza ubora na uwezo wake wa kuwa zana ya kumsaidia mwanafunzi.

Kamusi mbili zilizochambuliwa (KSKK na KKK) zote zimeonyesha kategoria za maneno ya Kiswahili. KSKK imeonyesha kategoria hizo kwa vifupisho vya Kiingereza kama vile n = noun; v = verb; a= adjective; adv =adverb. KKK imeonyesha vifupisho hivyo kwa Kiswahili kama *nm* = nomino; *kt* = Kitenzi; *kv* = Kivumishi, *ku* = Kiunganishi, *kw* = kiwakilishi nk. Kutofautiana huku katika kuonyesha vifupisho kunaweza kuashiria kuwa pengine hata walengwa wakuu wa kamusi hizi wanatofautiana kwa kiasi fulani. KSKK inaelekea iliwalenga wageni waliokuwa wanaingia katika maeneo ambapo Kiswahili kilizungumzwa na ndiyo maana maelekezo mbalimbali yametolewa kwa Kiingereza ambapo KKK inawalenga zaidi watumiaji wenye ufahamu wa Kiswahili na hivyo kutaka kupanua uelewa wao wa lugha ya Kiingereza na ndiyo sababu ya kutoa maelekezo kwa Kiswahili.

3.3.5 Etimolojia

3.3.5.1 Asili

Kamusi zote mbili zimeonyesha etimolojia za vidahizo vilivyoingia katika Kiswahili kutoka lugha nyingine. KSKK inaonyesha kuwa maneno mengi yaliyoingia yanatokana na lugha za Kiarabu, Kiajemi, Kihindi na yamewekewa alama ya nyota (*) na pia kuonyesha yanavyoandikwa kwa Kiarabu. Vivyo hivyo KKK nayo imeonyesha maneno yanayotokana na lugha zingine na kuwekea alama ya nyota (*) na mwishoni wa kila kidahizo lugha asili ya neno hilo kuandikwa kwa kifupi. KSKK imechangiwa na lugha zisizozidi sita ambazo ni Kiarabu, Kihindi, Kiajemi, Kituruki, Kiingereza na Kireno. KKK imechangiwa na zaidi ya lugha 12 nazo ni Kiarabu, Kihindi, Kiajemi, Kituruki, Kiingereza, Kireno, Kilatini, Kijerumani, Kihispania, Kifaransa, Kiibrania na Kichina. Katika kamusi zote mbili Kiarabu ndicho kimechangia msamiati mwingi zaidi hususan katika nyanja za utamaduni yaani msamiati wa vyakula, mavazi, dini ya kiislamu, miti na dawa za miti shamba. Kiingereza ndiyo lugha ya pili katika kuchangia msamiati wa lugha ya Kiswahili hususan katika nyanja za dini ya kikristo, maneno mengi ya sayansi na teknolojia. Lugha zilizobaki zimechangia maneno machache kila moja. Hii inadhihirisha jambo moja muhimu, nalo ni kuwa katika miaka ya hivi karibuni Kiswahili kimechota maneno mengi yanayowakilisha dhana mbalimbali toka lugha mbalimbali hususan katika sayansi na teknolojia ili kukidhi mahitaji ya kimsamiati katika karne hii ya ishirini na moja. Kuonyesha lugha asili ya neno lililoingia katika matumizi ya Kiswahili kunasaidia kuonyesha historia ya kukua na kupanuka kwa msamiati wa lugha.

**3.3.5.2 Maneno Husiani**

Maneno husiani ni maneno ambayo yapo katika kikoa kimoja cha maana yaani yenye uhusiano ingawa siyo wa karibu sana kimaana na kidahizo katika kitomeo kama ulivyo uhusiano baina ya visawe. Maneno husiani yanatolewa katika kitomeo ili kutoa ufahamu zaidi kwa mtumiaji wa kamusi. KSKK imeonyesha maneno ya aina hiyo kama katika mfano ufuatao:

**Kupia,** v. (1) wink, blink the eye; (2) nod from drownsiness. (Cf. ***pesa, kopesa, pepesa.***(KSKK, uk.230)

Maneno *pesa, kopesa* na *pepesa* yana maana zinazokaribiana ingawaje siyo visawe. Uingizaji wa maneno katika mtindo huu wa kikoa kimoja cha maana haukufanywa katika KKK. Kwa hiyo tunaweza kusema kuwa kwa kuzingatia kipengele hiki KSKK imemrahisishia zaidi mtumiaji anayejifunza Kiswahili kuweza kufahamu maneno yanayohusiana na neno analolitafuta ndani ya kamusi.

### 3.3.6 Fasiri

#### 3.3.6.1 Fasiri za maneno

Kamusi zote mbili zimezingatia kipengele cha kutoa fasiri kama njia mojawapo ya kufafanua maana ya kidahizo kinapokosekana kisawe cha lugha lengwa. KSKK imetoa fasiri hata pale ambapo neno moja la Kiingereza lingefaa. Hata hivyo ni njia mojawapo ya kukazia maana ili msomaji aweze kuipata dhana inayokusudiwa kwa usahihi zaidi. KKK imezingatia kuwa kisawe kimoja au zaidi kinapopatikana ndicho kitumike bila maelezo ya ziada. Hata hivyo faida ya ziada ya kutoa maelezo mbali na zilizotajwa hapo juu ni kwamba maelezo huchangia katika kupanua ukubwa wa kamusi.

#### 3.3.6.2 Mifano/ Muktadha

Kamusi zote mbili zimezingatia kutoa mifano kwa baadhi ya matumizi ya maneno. KSKK inatumia kidahizo kizima kwenye mfano wakati KKK inatumia alama ya kiwimbi (~) tu kama katika mifano ifuatayo:

**Haja*** n. (1) need, want, appeal for aid, request; (2) reason, cause, ground, excuse, claim, right; (3) what is needed ...
*Toa haja. kwa, Taka haja kwa* make a request to (KSKK, uk. 123).

Kidahizo haja kimerudiwa chote au neno haja limerudiwa lote katika mfano wa *Toa haja kwa, taka haja kwa*. Katika KKK kidahizo hicho kimeshughulikiwa kama ifuatavyo:

> **haja** nm [i-/zi-] 1 need, want, requirement, necessity, suit, request. 2 reason, ground. 3 call of nature: *Enda ~ kubwa* excrete; *Enda ~ ndogo* urinate.(KKK, uk. 96)

Mtindo wa kutumia kiwimbi (~)kwenye mifano unasaidia kupunguza ukubwa wa kitomeo. KSKK ina mifano mengi na yenye maelezo marefu wakati KKK ina mifano michache yenye maelezo mafupi. Hii ni moja ya sababu iliyochangia tofauti ya ukubwa kati ya kamusi hizi mbili.

#### 3.3.6.3 Alama za Uwanda Maalum

Kamusi zote mbili hazikubainisha maneno yanayotumika katika uwanda maalumu tu ikizingatiwa kuwa kamusi hizi zilitayarishwa kwa ajili ya matumizi ya jumla na siyo ya uwanda maalum. Hata hivyo kamusi ya Kiswahili – Kingereza ya TUKI imebainisha maneno machache sana yenye matumizi katika uwanda maalum kama

uwanda wa dini, (uislamu au ukristo), uwanda wa mambo ya bahari n.k kama katika mifano ifuatayo:

**chewa**[2] *nm* [*zi-*] (baharini) morning easterly winds.(KKK,uk.45)

**rakaa*** *nm* [*i-/zi-*] (Waislamu) bow (Kar) (KKK,uk.276)

**shirik.i**[2]* kt [*ele*] ( Ukristo) receive Holy Communion. (Kar) (KKK, uk. 292).

**3.3.7 Pragmatiki**

Vipengele muhimu vinavyoangaliwa katika pragmatiki ni hivi vifuatavyo. Kwanza, ni tahadhari za matumizi ya maneno yaani kumwongoza mtumiaji kutumia neno fulani mahali panapostahili na kwa hadhira inayostahili. Pili, alama za rejesta ili kueleza kuwa neno fulani ni rejesta ya mahali gani. Tatu, alama za kijiografia zinaonyesha mahali maneno yanapotumiwa zaidi katika eneo linalotumia lugha hiyo. Nne, utangamano ambao huonyesha maneno gani huendana pamoja katika sentensi. Vipengele vyote hivi vinne havikuonyeshwa katika Kamusi hizi mbili.

**3.3.8 Uhusiano**

**3.3.8.1 Kinyume**

Kinyume ni mbinu mojawapo inayoweza kutumiwa katika kutoa maana za maneno kwa kulieleza neno kwa kutumia neno ambalo ni kinyume cha lile linaloelezwa (Manser 1997). Kamusi zote mbili hazikufafanua maana za maneno kwa kutumia kinyume cha maneno.

**3.3.8.2 Istilahi Husiani**

Istilahi husiani ni maneno ambayo ni ya taaluma maalum na ambayo hutumiwa kuelezea kidahizo ambacho ni neno la kawaida. Kamusi ya KKK haikufasiri maana za maneno kwa kutumia istilahi husiani kama ambavyo KSKK imefanya katika baadhi ya vitomeo ambamo neno la kitaalamu limetolewa kama katika mifano ifuatayo:

> **Mkarakala**, n. mi- a timber-*tree Bridelia* sp., generally an indicator of soil, also *mkarati* and *mtututu* (KSKK, uk. 284).
>
> **Mkingu,** n. mi- a lac- bearing tree, *Albizzia lebbek* (KSKK, uk. 285).

Katika KKK vidahizo vilivyoambatana na istilahi husiani ni vile vya maneno yanayotaja miti na mimea.

**4. 0 Hitimisho**

Makala hii imechambua vipengele vilivyoshughulikiwa katika kamusi mbili za Kiswahili–Kiingereza. Uchambuzi umeonyesha kuwa kuna vipengele ambavyo kamusi zote mbili za Kiswahili–Kiingereza zilivishughulikia na vingine ambavyo havikushughulikiwa. Ulinganifu umefanywa kufuatana na mtazamo wa Nkwenti – Azeh (1995) unaozingatia vipengele vinane na ndani ya hivyo kuna vipengele vidogo 19. Hata hivyo, vipengele vya visawe kamili na visawe hafifu viliunganishwa na

kuwa kipengele kimoja. Hii ikafanya kuwe na vipengele 18.Pamoja na vipengele hivi kuna vipengele viwili vilivyoongezwa ambavyo ni ngeli za nomino na uelekezi na hivyo kuongeza idadi ya vipengele vilivyochambuliwa katika kamusi hizi mbili kufikia 20. Kati ya vipengele hivyo 20, KSKK iliingiza vipengele 13 na haikushughulikia vipengele 7 ambapo KKK imeingiza vipengele 10 na haikuingiza vipengele 8. Vipengele 2 viliingizwa kidogo. Kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wake, KKK imeingiza vipengele viwili yaani ngeli za nomino na uelekezi ambavyo vimeshughulikiwa kwa mapana zaidi kwa mara ya kwanza katika kamusi za Kiswahili – Kiingereza.

Kuingizwa kwa ngeli za nomino, na uelekezi katika kubainisha vitenzi kwenye KKK kunaifanya kamusi hii kuwa nyenzo bora zaidi ya mtumiaji kwani inamwongoza na kumwelekeza mtumiaji katika matumizi sahihi zaidi.

Uchambuzi huu umebainisha kuwa umbo la kitomeo linategemea aina ya walengwa wa kamusi. Kwa kamusi za Kiswahili kuna vipengele muhimu ambavyo kama havikuingizwa huifanya kamusi kutokidhi mahitaji ya watumiaji wake mbalimbali hasa inapokuwa kamusi ya jumla kama zilivyo kamusi hizi mbili zilizochambuliwa. Vipengele hivyo ni pamoja na kategoria za maneno, viambishi vya wingi, ngeli za nomino, minyambuliko ya vitenzi, uelekezi, asili ya maneno, visawe, fasiri na mifano. Hivi tunaweza kuviita vipengele vya msingi. Vipengele vya kinyume, istilahi husiani, vibadala, alama za uwanda maalum, alama za rejesta na alama za kijiografia, ni vipengele vya ziada. Ni ukweli usiopingika kuwa watumiaji wengi wa kamusi wanatafuta maana za maneno, lakini pia wapo wanaotafuta taarifa nyingine zaidi ya maana na hao ni muhimu kuzingatia mahitaji yao pia. Makala hii inashauri kuwa kuingiza vipengele vingi katika kamusi kunaifanya kamusi kuwa nyenzo bora zaidi kwa watumiaji wake.

Kutokana na hali hiyo, umuhimu na uamuzi wa kuingiza au kuacha vipengele kadhaa vya ziada baada ya vipengele vya msingi kushughulikiwa unaweza kufanywa kwa makusudi na wasawidi kamusi. Hili linawezekana kutegemea walengwa wa kamusi inayokusudiwa kwani itakuwa vigumu kuingiza kila kipengele katika kila kitomeo katika kamusi ya jumla kama zilivyo kamusi hizi mbili. Hali hiyo inawezekana tu kwenye kamusi kubwa za aina ya saiklopidia.

## MAREJEO


Berube, S. M (1998), Children's *Dictionary*, Houghton Mifflin, USA.

Chuwa, A.R. (2001), Junior *English – Swahili*, BPL Publishers, a Division of Business Printers Ltd, Dar es salaam.

Crystal, David. (1991), *A Dictionary of Lingustics and Phonetics*, Blackwell Publishers, UK.

Harris, Roy (1973), *Synonymy and Linguistic Analysis*, University of Toronto Press, Toronto, Canada.

Kihore, Y.M. na wenzake (2001), *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*, TUKI, University of Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Jackson, Howard (1988), *Words and Their Meaning*, Longman, London.

Johnson, Frederick (2000), *A Standard Swahili – English Dictionary*, Oxford University Press, Dar es Salaam & Nairobi.

Manser, Martin H. (1997), *Chambers Dictionary of Synonyms and Antonyms*, Chambers Harrap Publishers, Edinburgh, UK.

Nkwenti- Azeh, B. (1995), *'The Treatment of Synonymy and Cross*-Reference in Special – Language Dictionaries (SLD$^{S}$)' *Teminology* 2:325- 50.

Olivera, Pedro A. Fuertes and Marisol Velasco –Sacristan, 'A Critical Comparison of macrostructure and microstructure of Two Bilingual English- Spanish Dictionaries of Economics' katika Cowie, A. P. (mhariri), (March, 2001) *International Journal of Lexicogra*phy *Juzuu 14. Na 1*, Oxford University Press: 13-55.

Singh, Ram Adhar (1982), *An Introduction to Lexicography*, Central Institute of Indian Languages, Manasagangotri, Maysore, India.

TUKI, (1981), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

TUKI, (2001), *Kamusi ya Kiswahili – Kiingereza*, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

**UFAFANUZI WA VIFUPISHO**

tde = Kinyambuo tendea
tden = Kinyambuo tendeana
tdk = Kinyambuo tendeka
tdn = Kinyambuo tendana
tds = Kinyambuo tendesha
tdew = Kinyambuo tendewa
tdw = Kinyambuo tendwa.

Prep = Prepositional (tendea)
St = Stative (tendeka)
Cs = Causative (tendesha)
Ps = Passive (tendwa)
Pot = Potential (tendeka)
Rp = Reciprocal (tendana)
nm = Nomino
kt = kitenzi
v = Verb (kitenzi)
n = Noun (nomino)
ki = Kiingizi (interjection)
Kaj = Kiajemi (Persian)
Kar = Kiarabu ( Arabic)
Cf = Compare (Linganisha)